JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA

ISSN 0856 - 4965 | TOLEO NO. 13 | OKTOBA - DESEMBA 2025

# JARIDA LA TAFORI



TANZANIA NA CHINA ZABAINI FURSA ZA USHIRIKIANO KATIKA UTAFITI WA MISITU NA UFUGAJI NYUKI

TAFORI YAFANYA UTAFITI KUBAINI MCHANGO WA MIANZI KATIKA KUBORESHA AFYA YA UDONGO

TAFORI YASHIRIKI MKUTANO MKUU WA CITES 2025 NCHINI UZBEKISTAN

JARIDA HILI HUTOLEWA NA KUSAMBAZWA NA TAFORI

@taforitz | www.tafori.or.tz





# UJUMBE KUTOKA KWA

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | **TAFORI**


**Mpendwa Msomaji**

Napenda kuchukua nafasi hii kukukaribisha tena kwenye toleo letu la Oktoba 2025 la Jarida lako pendwa la Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI). Jarida hili huchapishwa mara nne kwa mwaka. Wachangiaji katika Jarida hili ni watafiti na wadau wengine wa misitu na nyuki ambao wanataarifa au makala muhimu kwa ajili ya kuelimisha jamii.

Toleo hili linakuletea taarifa mbalimbali zinazohusiana na utafiti wa misitu na ufugaji nyuki lakini pia na Serikali ilivyojipanga kuimarisha uwezo wa TAFORI ili kutoa huduma bora na kuboresha utafiti wa rasilimali za misitu na nyuki. Miongoni mwa taarifa zilizomo ndani ya toleo hili ni Tanzania na China zilivyobaini fursa za ushirikiano katika utafiti wa misitu na ufugaji nyuki, TAFORI ilivyoshiriki mkutano mkuu wa Cites 2025 nchini Uzbekistan, pamoja na TAFORI na TAWIRI zilivyoshirikiana kufanya utafiti wa bayoanuai katika misitu ya hifadhi ya Essimingori, Nou na Hasama kwa ajili ya uwekezaji wa utalii.

Nipende kutoa shukrani za pekee kwa Waandishi wote walioandaa makala kwa ajili ya Jarida hili. Aidha shukrani ziwafikie pia Wahariri wote kwa kazi yao nzuri ya kuhariri na kuhakiki makala za Jarida hili.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la TAFORI.



Dkt. Revocatus Mushumbusi

**MKURUGENZI MKUU**

**TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA (TAFORI)**



# YALIYOMO

**Uhariri**
**Mhariri Mkuu**
Dkt. Revocatus Mushumbusi
**Mhariri Mtendaji**
Dkt. Joshua Maguzu

**Wahariri**
Dkt. Siwa Nkya, Dkt. Nancy Pima,
Dkt. Elisha Njoghomi, Bw. Stanslauss Lukiko
**Mhariri Msaidizi**
Bw. Davis Kiwelu, Bi. Lucy Akwilini

**Linatolewa na kusambazwa na:**
Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania
S.L.P 1854, Morogoro
Simu: +25523 2935174/2935177
Nakushi: +255 23 2935174
Barua pepe: tafori@tafori.or.tz
Tovuti: www.tafori.or.tz

Neno Kutoka kwa Mhariri Mkuu .......... 2

Tanzania na China Zabaini Fursa za Ushirikiano Katika Utafiti wa Misitu na Ufugaji Nyuki .......... 4

TAFORI Yashiriki Mkutano Mkuu wa Cites 2025 Nchini Uzbekistan .......... 5

TAFORI Yaanza Utafiti wa Kuzalisha Miche ya Mgunga .......... 6

TAFORI na TAWIRI Zashirikiana Kufanya Utafiti wa Bayoanuai Katika Misitu ya Hifadhi ya Essimingori, Nou na Hasama kwa Ajili ya Uwekezaji wa Utalii .......... 7

TAFORI Yafanya Utafiti Kubaini Mchango Wa Mianzi Katika Kuboresha Afya ya Udongo .......... 10

Uthakili wa Mti Jamii ya Syzygium (Mzambarau)Miongoni mwa Wazanaki Mkoani Mara. .......... 12

**MATANGAZO**
Forestry Researchers Registration Application Form .......... 15

Usajili kwa Watafiti na Miradi ya Utafiti .......... 16

Kumbi za Mikutano .......... 18

**Limesanifiwa na:**
Bw. Davis Kiwelu

**Jarida hili huchapishwa mara nne kwa mwaka na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI).**

**Lugha:** Lugha inayotumika katika Jarida hili ni Kiswahili

**Walengwa:** Wadau katika sekta za misitu na ufugaji nyuki

**Malengo:** Jarida hili huchapishwa ili:-

1. Kuhabarisha na kuelimisha umma kupitia tafiti mbalimbali zinazofanywa na kuratibiwa na taasisi.
2. Kutumika kama jukwaa la mawasiliano baina ya watafiti na wadau wa sekta ya misitu na ufugaji nyuki.

# Tanzania na China Zabaini Fursa za Ushirikiano Katika Utafiti wa Misitu na Ufugaji Nyuki

**Dodoma.** Serikali ya Tanzania kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na ujumbe wa wataalamu wa misitu kutoka Jimbo la Hunung, China wameanza majadiliano ya kuimarisha ushirikiano wa kitaalamu katika tafiti, uhifadhi na kukuza utalii wa misitu.




Ujumbe huo kutoka Jimbo la Hunan, ambao uko nchini kwa ziara maalumu, ulitembelea TAFORI Novemba 13, 2025, kwa lengo la kufahamu majukumu ya Taasisi na kutambua maeneo yenye fursa za ushirikiano wa kisayansi.

Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI, Dkt. Revocatus Mushumbusi, alisema Taasisi yake imejikita katika kufanya tafiti za misitu na ufugaji nyuki, kuhifadhi taarifa za rasilimali za kiasili na kubuni teknolojia za kuongeza tija katika usimamizi wa misitu, hivyo iko tayari kushirikiana na China katika maeneo ya utafiti, uvumbuzi na uhamishaji teknolojia.

Naye Mkurugenzi wa Utafiti wa Misitu TAFORI, Dkt. Chelestino Balama, alieleza kwa undani kazi za taasisi hiyo, akitaja fursa za mashirikiano kama kuanzisha bustani za mimea, tafiti za pamoja za spishi adimu za miti zilizohatarini kutoweka duniania, na kubadilishana taarifa za kisayansi kati ya taasisi hizo mbili.

Kwa upande wa ujumbe wa Jimbo la Hunung, China, kiongozi wa msafara ambaye pia ni Mkurugenzi wa Idara ya Misitu Jimbo la Hunung, Jianga Rui, alisema wamelenga kujifunza mifumo ya uhifadhi ya Tanzania na kutafuta miradi ya pamoja itakayojenga uhusiano wa kirafiki na kukuza utafiti, uhifadhi na utalii wa misitu.

Alisema baada ya kurejea China, watapeleka taarifa kwa mamlaka husika ili kuratibu maandalizi ya rasimu ya makubaliano yatakayowezesha kuanza kwa hatua za ushirikiano.





# TAFORI Yashiriki Mkutano Mkuu wa Cites 2025 Nchini Uzbekistan

**Samarkand, Uzbekistan.** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imeshiriki kikamilifu katika Mkutano wa 20 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora - CITES CoP20), kuanzia Novemba 24 hadi Disemba 5, 2025, jijini Samarkand, nchini Uzbekistan.

Mkutano huo, ulihudhuriwa na zaidi ya washiriki 3,000 kutoka nchi wanachama 160, ukihusisha Taasisi za Kiserikali na wadau wa Maendeleo. Tanzania iliwakilishwa na ujumbe kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Idara ya Wanyamapori, TAFORI, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

Akifungua mkutano huo Bw. Aziz Abdukhakimov Mgeni rasmi na Mshauri wa Rais wa Uzbekistan kuhusu Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Ikolojia na Mabadiliko ya Tabianchi alisisitiza nchi wananchama kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira, kupanua maeneo yaliyohifadhiwa na kukabiliana na biashara haramu ya wanyamapori na mimea.

Akiangazia mageuzi ya hivi karibuni nchini Uzbekistan ambayo yameweka uhifadhi wa mazingira kama kipaumbele kwa Serikali, alitoa wito kwa washiriki kutumia teknolojia, ikiwemo Akili Unde (AI) katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uhifadhi na biashara ya wanyamapori na mimea.

Mkutano wa CoP20 ulijadili ajenda 114 na mapendekezo 51 yanayohusu spishi mbalimbali kama tembo, chui, fisi, papa, taa, mijusi, majongoo bahari, vinyonga, pamoja na miti ya thamani kama vile mpingo, mninga na mkongo. TAFORI katika kutimiza jukumu lake kama Mamlaka ya Kisayansi ya CITES ilichangia mijadala muhimu kuhusu usimamizi endelevu na ulinzi wa spishi za mimea.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TAFORI, Dkt. Revocatus Mushumbusi alishiriki katika mkutano huu akiambatana na Mkurugenzi wa Utafiti, Dkt. Chelestino Balama ambaye huiwakilisha Tanzania katika Kamati ya Mimea ya CITES kama mjumbe kutoka Kanda ya Afrika. Katika Mkutano huo TAFORI ilitoa mchango mkubwa katika kujadili, kuunga mkono ajenda na mapendekezo kuhusu spishi za mimea ambazo zimeonekana kuwa na maslahi mapana kwa nchi.

Ushiriki wa TAFORI katika Mkutano huu ulikuwa muhimu katika kuimarisha msimamo wa pamoja wa Tanzania kwa baadhi ya ajenda hasa katika mijadala ya kanda ya Afrika na kuendelea kutetea maslahi mapana ya nchi katika maeneo ambayo nchi inanufaika na biashara ya kimataifa kupitia maliasili za wanyamapori na mimea.



# TAFORI Yaanza Utafiti wa Kuzalisha Miche ya Mgunga

**Siha, Kilimanjaro.** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) imeanzisha utafiti wa kubaini mbinu bora, rahisi na za haraka za uoteshaji na uzalishaji wa miche ya Mgunga (*Acacia tortilis*) katika vitalu vya miti. Hii ni kutokana na changamoto ya ugumu wa magamba ya mbegu za miti ya mgunga ambayo imekuwa kikwazo kikubwa katika uzalishaji wake kwa wingi.



Aidha, utekelezaji wa utafiti huu unatarajiwa kuboresha upatikanaji wa miche ya mgunga na kuunga mkono juhudi za kurejesha uoto wa asili uliopotea katika maeneo yaliyoathiriwa na uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za binadamu, ikiwemo ukataji miti hovyo, ongezeko la mifugo na kuenea kwa mimea vamizi.

Matokeo ya utafiti huu yatawezesha TAFORI kuandaa mwongozo rasmi wa kitaalamu wa njia bora na za haraka za uoteshaji wa mbegu za mgunga, ambao utawanufaisha jamii, taasisi na wadau wa uhifadhi katika kuanzisha vitalu vya miche na kuchangia kurejesha na kuimarisha uoto wa asili nchini.









# TAFORI na TAWIRI Zashirikiana Kufanya Utafiti wa Bayoanuai Katika Misitu ya Hifadhi ya Essimingori, Nou na Hasama kwa Ajili ya Uwekezaji wa Utalii

Timu ya watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti Misitu Tanzania (TAFORI) na Taasisi ya Utafiti wa Wanayamapori Tanzania (TAWIRI) zashirikiana kufanya utafiti wa Bayoanuai katika misitu ya hifadhi ya Essimingori, Nou, na Hasama kwa ajili ya uwekezaji wa utalii. Lengo la utafiti huu likiwa ni kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kukuza sekta utalii kwa kuongeza vyanzo vya utalii nchini.

Watalii watapata fursa ya kuona na kujifunza mimea, wadudu, ndege, na wanyama wa aina mbalimbali wanaopatikana kwenye misitu hii Mitatu ya hifadhi. Pia watalii wataweza kuona sehemu mbalimbali za kufanyia ibada ndani ya misitu ya hifadhi pamoja na kuona madhari nzuri.

# #TAFORI TUNATEKELEZA

# TAFORI Yafanya Utafiti Kubaini Mchango wa Mianzi Katika Kuboresha Afya ya Udongo



## UTANGULIZI

Mianzi ni miongoni mwa rasilimali muhimu za misitu zenye mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira na uboreshaji wa afya ya udongo. Mbali na matumizi yake ya kiuchumi kama vile ujenzi, nishati, na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali, mianzi ina nafasi ya kipekee katika kuimarisha afya ya udongo na kupunguza mmomonyoko. Hii inatokana na mfumo wake imara wa mizizi mingi iliyoshikana ardhini pamoja na uzalishaji mkubwa wa masalia ya mianzi (Majani, vijiti na magome). Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kupitia Kituo cha Utafiti wa Misitu Kibaha (KLAFC) kimefanya utafiti wa kutathmini mchango wa spishi za mianzi katika uhifadhi wa udongo, kuboresha muundo wa udongo na kuongeza rutuba kwa njia za asili.

Katika utafiti huu, spishi za mianzi zilizotathminiwa ni *Dendrocalamus membranaceus, Bambusa vulgaris* na *Bambusa balcooa*. Spishi hizi zilichaguliwa kwa sababu zinapatikana kwa urahisi, zinastawi vizuri katika mazingira ya Tanzania, na zinawakilisha aina muhimu za mianzi zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha masalia yanayochangia uboreshaji wa afya ya udongo. Shughuli kuu za ukusanyaji wa data katika utafiti huu zinahusisha ufuatiliaji wa kuanguka kwa majani na masalia ya mianzi pamoja na kasi ya kuoza kwa masalia ya mianzi kama majani na magome kwenye udongo.

Matokeo ya awali yanaonesha kuwa mianzi ina mchango chanya katika kuboresha afya ya udongo kupitia kuongeza mabaki ya kikaboni, kuhifadhi unyevunyevu na kupunguza mmomonyoko wa udongo. Kutokana na manufaa hayo, wananchi wanashauriwa kuzingatia upandaji wa mianzi kama sehemu ya juhudi za kuhifadhi mazingira na kuboresha rutuba ya udongo kwa njia endelevu.

## KUANGUKA KWA TAKATAKA ZA MIMEA NA UMUHIMU WAKE KWA RUTUBA YA UDONGO

Kudondoka kwa majani ni mchakato wa asili ambapo majani, matawi madogo, magome, na masalia mengine ya mimea huanguka na kufunika uso wa udongo.Matokeo ya awali upande wa *litter fall, Bambusa balcooa* ilionyesha kiasi kikubwa zaidi cha udondoshaji wa majani, vijiti, magome na masalia mengine ikifuatiwa na *Bambusa vulgaris* na kisha *Dendrocalamus membranaceus*.

## KASI YA KUOZA KWA MASALIA YA MIANZI NA MZUNGUKO WA VIRUTUBISHO

Kasi ya kuoza kwa masalia ya mianzi inapitia mchakato wa kuvunjwa kwa masalia hayo, kuoza, na hatimaye kutoa virutubisho kwenye udongo. Kila spishi ilichukuliwa sampuli 8 zenye ujazo wa gramu 40 kila moja ambapo zilizikwa kwenye shimo la urefu wa sentimita 60 na upana sentimita 100. Matokeo ya awali ya kasi ya kuoza kwa aina tatu za mianzi kwa kuzingatia magome



na majani, *Dendrocalamus membranaceus* na *Bambusa vulgaris* zimeonesha wastani wa juu zaidi wa kasi ya kuoza kwa mwezi upande wa magome. Hali kadhalika, upande wa majani, *Dendrocalamus membranaceus* imeonesha wastani wa juu zaidi wa kasi ya kuoza kwa mwezi, ikifuatiwa na Bambusa vulgaris huku *Bambusa balcooa* ikiwa na kasi ya chini zaidi..

## HITIMISHO

Utafiti umeonesha kuwa mianzi ina mchango mkubwa katika kuboresha afya ya udongo kupitia uzalishaji wa masalia na kasi ya kuoza kwake. Matokeo yanaonesha kuwa *Bambusa balcooa* huzalisha kiasi kikubwa zaidi cha masalia kama majani na matawi, hivyo kuwa muhimu katika kuhifadhi unyevunyevu wa udongo na kupunguza mmomonyoko kwa muda mrefu. Aidha, *Dendrocalamus membranaceus* pamoja na *Bambusa vulgaris* zimeonesha kasi ya juu zaidi ya kuoza kwa masalia yake, jambo linalochangia kurudisha virutubisho udongoni kwa haraka na kuongeza rutuba kwa ufanisi. Hivyo basi, uteuzi wa spishi ya mianzi unapaswa kuzingatia lengo la matumizi:

*Bambusa balcooa* inapendekezwa kwa matandazo ya muda mrefu na udhibiti wa mmomonyoko, wakati *Dendrocalamus membranaceus* na *Bambusa vulgaris* zinafaa zaidi kwa uzalishaji wa mboji ya haraka na uboreshaji wa rutuba ya mazao. Utafiti huu unaweka msingi muhimu wa matumizi endelevu ya mianzi katika usimamizi wa udongo na kilimo himilivu.









*Imeandaliwa na Joseph J. Chogga, Nancy E. Pima, Stella C. Ntayomba na Ibrahim Hussein*

# Uthakili wa Mti Jamii ya Syzygium (Mzambarau) Miongoni Mwa Wazanaki Mkoani Mara.

## UTANGULIZI

Mti wa mzambarau unaojulikana kibotania kama *syzygium* ni miongoni mwa jamii ya mti inayopatikana zaidi katika sehemu nyingi za nchi. Mzambarau ni mti wa matunda, na matunda yake huitwa zambarau, pia kwa kawaida ni mti wa nyumbani.

Kuna aina mbalimbali za spishi ya *syzygium* katika mazingira yetu lakini zinazojulikana zaidi ni pamoja *Syzygium guineensee*, *Syzygium cordatum, Syzygium cumini (S.jambolanum)* na *Syzygium owariense.* Hata hivyo kwa watanzania wengi mti huo unajulikana tu kama mzambarau bila kujali aina zake, kwa kuwa kutofautisha aina moja ya mti wa mzambarau na mwingne ni vigumu. Inafahamika, ingawa inaweza isiwe rahisi kwa mtu ambaye si mtaalamu (wa jadi au mwanabotania) kutofautisha sifa za aina moja na nyingine.

Kwa mfano ukiangalia gome la *S.cordatum* unaweza kukuta kuwa ni tofauti na *S.cumini* ambalo ni rangi ya kahawia iliyokolea lenye mabaka na nyufa ambapo gome la *S.cumini* ni la rangi iliyokolea na lenye mabaka kwenye shina, nyororo na rangi hafifu kwenye matawi machanga. Vile vile aina nyingine mbili ambazo ni *S. guineensee, S.owariense* ambazo sifa zake, ni za kijivu au kijivu iliyokolea zenye mabaka na zinazo menyuka kadiri umri uanavyoongezeka kwa ile ya mwisho, mbali na sifa za gome lakini pia hutofautiana kwenye majani, matunda na maua. Sifa hizo zinaweza zisiwe dhahiri sana kwa mtu wa kawaida.

Utafiti wa kitaalamu unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 99 ya miti ya mzambarau inayopatikana nchini ni miti mwitu iliyoota kwa bahati mbaya, yaani iliyoota yenyewe na kutawanyika hapa na pale katika maeneo ya mijini na vijiji.

Aina ya mti wa mzambarau pia inaonekana kuwa kati ya aina chache sana za miti ambayo inaonekana kukaidi vizuizi vya kijiogorafia pamoja na hali ya hewa kwa kuwa mtu anaweza kupata mti wa mzambarau karibu sehemu zote za nchi.

## SIFA ZA MATUNDA YA ZAMBARAU NA HADITHI ZILIZOPO;

Tunda la zambarau lina sifa zifuatazo za lishe; Ni tamu lina virutubisho na hutoa faida za kiafya za kuvutia lina sifa dhabiti za kuzuia uvimbe, huboresha sukari ya damu na mwitikio









wa insulini na pia hutoa faida nyingine kwa afya ya moyo, ikiwa ni pamoja na kuboresha utendaji wa mishipa ya damu. Faida nyingine za lishe ni pamoja na kuwa na ngozi nzuri na kulinda dhidi ya saratani ya koo, mdomo, matiti na utumbo mpana Beri zote zikiwemo zambarau zinafanana kiasi katika maudhui ya vitamini na madini. Kwa kuongezea sifa hizo za zambarau kama zilivyoelezwa hapo juu, matunda ya mzambarau ambayo yanajulikana kama zambarau pia ni maarufu sana miongoni mwa watoto.

Hata hivyo licha ya matunda ya mzambarau kuwa matamu, jamii ya mti wa mzambarau imezungukwa na hadithi za kitamaduni au za jadi na siri ambazo haziwezi kuthibitishwa kisayansi. wa mfano, wakati katika eneo la pwani la Tanzania, mti wa mzambarau unahusishwa na kuwepo kwa mapepo na majini wengine wabaya. Katika maeneo ya bara mti huo pia unachukuliwa kuwa jamii ya mti uliolaaniwa. Miongoni mwa watu wa zanaki kwa mfano, jamii ya mti wa mzambarau inachukiwa sana. katika vijiji 7 vya butiama (Makore, Nyamegembe, Ikorokomyo, Ntuzu, Kitanga, Muhunda na Butesya) vinazunguka hifadhi ya msitu wa Mwalimu Nyerere wa Muhunda huko Mwitongo, wilaya ya Butiama mkoani Mara, kwa mfano imani potofu kama hiyo ilitawala sana miongoni mwa watu.

Inaonekana kuna imani potofu ya muda mrefu miongoni mwa watu wa Zanaki kwamba mti wa Mzambarau una mvuto usiyoweza kuzuilika kwa watoto na kwamba mara tu mtoto anapopanda mti wa mzambarau na kutokea kuanguka kutoka kwenye mti huo lazima apate matokeo mabaya ikiwa siyo kupoteza maisha na au wakati mwingine anaweza kupata ulemavu wa kudumu. Ni kwa sababu ya imani hiyo potofu kali katika uovu wa mzambarau kwamba watu wa zanaki sio tu wanajiepusha kabisa

na kupanda jamii ya mti wa mzambarau lakini pia hawapendi au hawaruhusu watu wengine kupanda jamii ya mti huo katika maeneo yao.

Kwa hivyo, haishangazi kwamba hata wakati miche ya miti ya bure ilitolewa kwa baadhi ya watu katika maeneo ya Musoma chini ya mradi wa uhifadhi wa Mwalimu Nyerere unaoendelea ,watu katika eneo la uhinda walikwepa au waliogopa miche ya hifadhi ya msitu wa Mzambarau.

## UKWELI KUHUSU JAMII YA MTI WA MZAMBARAU

Hakuna maelezo ya wazi ya kisayansi kuhusu hadithi iliyopo kwamba mara tu mtoto anapoanguka kutoka kwenye mti na baadaye kufa linahusishwa na roho mbaya haina msingi. Mtoto anaweza kuanguka kutoka kwenye mti mwingine wowote bila kujali jamii ya mti huo. Aidha, sababu za kwanini kuna visa vingi vya watoto kufa baada ya kuanguka kutoka kwenye mti wa mzambarau ni mbili; moja ikiwa urefu wa mti ambao ni takribani mita 25 juu na taji yake kufunika mita 10 au zaidi kwa upana. Pili kupoteza umakini miongoni mwa watoto mara tu wanapofika kwenye tunda la zambarau lenyewe. Sababu ya watoto kupoteza umakini kama huo ni kwamba wanakuwa wameelekeza mawazo yao kwenye tunda hilo kwa sababu ya ladha ya matunda ya zambarau na labda tamaa ya watoto ya kutaka kukusanya matunda mengi kwa muda mfupi.

## HITIMISHO

Licha ya imani potofu kuelekea jamii ya mti wa mzambarau, matunda yake ni chakula chenye afya kwa mwili wa binadamu. Inapendekezwa kuwa imani potofu kama hiyo inapaswa kuachwa mara moja.

Hata hivyo, ili imani hiyo potofu iachwe jamii hasa kundi la wazee (miaka 50 na zaidi) inapaswa kuhusishwa katika kuandaa mitaala ya kuongeza uelewa juu ya faida ya jamii ya mti wa mzambarau na kinyume na spishi fulani za miti mingine ambayo inashikiliwa kwa hofu kubwa na heshima na watu kama vile mbuyu na panga uzazu aina *Terminalia mantaly*, kutaja machache ambayo hayajumuishwi.

*Imeandaliwa na Estella Mbala, Iddy Dibwa, na Joshua Mfumbilwa*

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**
**TANZANIA FORESTRY RESEARCH INSTITUTE**

# APPLICATION FORM FOR REGISTRATION OF FORESTRY RESEARCHER

(Submit soft and hard copy)

**PART A**

Attach current passport size photo

1. Surname.........................................................................................
Other names......................................................................
Physical address ......................................................................
Email Address.......................................... Phone Number..........................
2. Citizenship:.................................... Country of origin:....................................
Institutional affiliation:..................................................................................
Mailing address (outside Tanzania):..........................................................................
3. Academic qualifications (Start with most current);
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
4. Referees' names and addresses (two referees preferably one of whom must be based in Tanzania)
(a) ..........................................................................................................
..........................................................................................................................................
(b) ..........................................................................................................
..........................................................................................................................................
5. Recent publications:
(a) ..........................................................................................................
(b) ..........................................................................................................
(c) ..........................................................................................................
(d) ..........................................................................................................
6. Society Membership (if any):
(a) ..........................................................................................................
(b) ..........................................................................................................
(c) ..........................................................................................................
7. Attach current curriculum vitae (CV) and certifies copies of academic certificates

Signature of the applicant ...................................................................... Date: ..........................

PART B

FOR OFFICE USE

Official stamp Official stamp

Research registration number ......................................................................
Recommendation..............................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
Signature .............................................. Date: ............................

***To be able to register online please visit out website: www.tafori.or.tz***



# Conference Halls Package

**From Tsh. 200,000 - Tsh. 800,000**

Conference Hall with Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water O.5Ltrs | Internet Connection and LCD - Projector





**Tsh. 300,000**

**NSHUBEMUKI MINI CONFERENCE HALL**

1 - 15 participants per Day

**Tsh. 600,000**

**MURIRA BOARD ROOM**

1 - 35 participants per Day

**Tsh. 800,000**

**SABAS CONFERENCE HALL**

1 - 70 participants per Day

Conference Hall include; Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water 0.5Ltrs | Internet Connection and LCD - Projector

# TAFORI Conference Halls

*Packages*







**Tsh. 200,000**

**NSHUBEMUKI MINI CONFERENCE HALL**

1 - 15 participants per Day

**Tsh. 500,000**

**MURIRA BOARD ROOM**

1 - 35 participants per Day

**Tsh. 700,000**

**SABAS CONFERENCE HALL**

1 - 70 participants per Day

Conference Hall include; Air Conditioner (AC) | Stationaries | Refreshment | Bottle of Water O.5Ltrs

**CONTACTS**

0223-29-351-76 | tafori@tafori.or.tz

TAFORI HQ Morogoro, P.O.Box. 1854 | Kingolwira Highway

Morogoro - Dar es Salaam

@taforitz | www.tafori.or.tz




# RESEARCHERS & PROJECT REGISTRATION

## REGISTRATION OF FORESTRY AND BEEKEEPING RESEARCHERS


### Services Requirements

Completer application form

Copy of higher education certificate

Payment receipt

Passport size photo







@taforitz | www.tafori.or.tz

# REGISTRATION PROCESS

## FEES AND OTHER CHARGES

| SN | RESEARCH ACTIVITIES | TANZANIAN RESEARCHER (TZS) | FOREIGN RESEARCHER (USD) |
|---|---|---|---|
| 1. | Researcher registration fees | 20,000 | 20 |
| 2. | Application fees for conducting research project | 20,000 | 100 |
| 3. | Registration fees for conducting research | | |
| | Student (Undergraduate) | Free | Free |
| | Student (Masters) | 30,000 | 100 |
| | Student (PhD) | 50,000 | 300 |
| | Post-Doctorate / Research fellow | 100,000 | 400 |
| | Individual Research | 200,000 | 500 |
| 4. | Extension of research | 30,000 | 100 |
| 5. | Export of specimens | 50,000 | 200 |
| 6. | Data access | 500,000 | 1000 |
| 7. | Scientific talks, lectures or seminars | 500,000 | 300 |

# REGISTRATION OF FORESTRY AND BEEKEEPING RESEARCH PROJECTS

- **Service Requirements**
- Research proposal
- Copy of the registration certificate as a researcher
- Completed application form
- Curriculum Vitae (CV)
- Signed form for adhering to procedures
- Identification letter from the Head of the Institution
- Letter from your sponsor
- Copy of Higher Education Certificate
- Payment receipt
- Passport-size photo
- Copy of NIDA identification for Tanzanians and passport for non-Tanzanians
- Name and letter of your project partner for non-Tanzanians



"Utafiti wa Misitu na Ufugaji Nyuki kwa Ustawi wa Uhifadhi na Maendeleo ya Viwanda"


**TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA - TAFORI**

Tel: +255 23 2935174 | Fax: +255 23 2935174

TAFORI HQ Morogoro, P.O.Box. 1854 | Kingolwira | Highway Morogoro - Dar es Salaam

Email: tafori@tafori.or.tz | Website: www.tafori.or.tz